*SWAHILI FORUM 30 (2023): 233-250*

# SIKU MOJA OFISINI
# NAFASI YA UPAPASI MJINI ZANZIBAR

MUCHI (MUSTAFA SALUM ABDULLA) NA BAHATI (IRENE BRUNOTTI)[1]

Tukizingatia kona maalum mjini Zanzibar, yaani ofisini, mtaani Shangani Posta, leo hii mimi na mwenzangu Muchi tunataka kuwahadithia kuhusu kikundi cha vijana wanaoitwa mapapasi ambao wamekuwa wanafanya kazi katika sekta ya utalii tangu miaka ya Themanini, japo nafasi yao haijawahi kutambuliwa wala kurasimishwa na serikali. Badala yake, mara nyingi vijana hao wamekuwa wanaudhiwa, kupuuzwa na kuadhibiwa kwa vile wanapwaya kwenye dira ya kiserikali ya kuigeuza Zanzibar kuwa mahali pa kutalii (kwa maana ya *touristic destination*) pakiingizwa kwenye mikondo mikali ya kiliberali mamboleo. Muchi na mimi tunajadiliana na kusimulia (hi)stori(a) yenye pande zaidi ya mbili. Tutawafafanulia kazi ya upapasi kama ilivyokuwa zamani na sasa hivi. Pia, tutatafakari juu ya nafasi ya upapasi (na uwenyeji) mjini Zanzibar, tukichambua maana, athari na uwezo wake. Hivyo, tutazingatia nafasi kama kielelezo cha au methodolojia ya kuchambua maneno ya Kiswahili kama vile yalivyo, lile linaloliwezesha, pamoja na maana yao. Umbo lenyewe la mazungumzo linasisitiza kuwa fikra zinazotokea kwenye mahusiano yanazaliwa konani, pale ambapo hakuna anayetiliwa (na kinachotiliwa) maanani kabla hajapewa (na hakijapewa) nafasi huko huko, nafasi ambayo hatimaye ndiyo ya Muchi na yangu pia.[2]

By exploring the microcosmos of a junction (kona) in the neighbourhood of Shangani Posta, in the city of Zanzibar, today Muchi and I will tell you the (hi)story of a unique segment of Zanzibari male urban youth, known as mapapasi, working in tourism since the 80s. While been neglected and denied an official, formal and legal recognition by the government, they have been continuously harassed, intimidated and shamed because perceived as not belonging, not fitting the governmental project of turning Zanzibar into a touristic destination. The following conversation aims at disclosing the complexity hidden behind the mainstream one-sided picture of them. Looking at the past and contemporary practices of upapasi, Muchi and I reflect on the nafasi of upapasi in urban Zanzibar and matter-forth upapasi (and uwenyeji as an instance of spatial il/legalization), their meaning and their doing. In this way, we are attentive to the wor(l)d nafasi, as analytical lens to get a sense – kusikia, kuona, kuwa na – urban Zanzibar. The very form of conversation is meant to think thoughts as they are co-constituted by and within the relationalites of the kona, whereas no-body is predetermined, rather every-body is co-constituted in the very situatedness in which also Muchi and I (be)come-with.

[1] Mazungumzo haya yalitokea hadharani mwa Baraza la Kiswahili la Berlin, tarehe 13 mwezi wa Juni, 2022. Haya ndiyo maandishi yanayotokana na majadiliano hayo yaliyokuwa yameitwa *Siku Moja Ofisini: Nafasi ya Upapasi Mjini Zanzibar* (*One Day at the Office: Mattering-forth Upapasi in Urban Zanzibar*). Kwa sababu tunavyojuana wenyewe kwa wenyewe tangu miaka ya Tisini tunaitana Muchi na Bahati. Hivyo ndivyo tulivyoamua kuitwa kwenye majadiliano na maandishi yake pia. Lengo letu ni kushirikiana na wasomaji mawazo yetu tukijaribu kuyaacha majadiliano vile yalivyojitokeza, bila kugusa mwendo wake wala mahadhi yake. Hata hivyo, tunafahamu kuwa kazi hii haiwezi kuwa sawasawa na ile; pengine hapo ndipo uwezo wake ulipo. Tunatumaini kazi hii ishawishi kazi nyingi nyenginezo zikifanywa kuanzia, kupitia na kuishia na mshikamano wa namna hii.

[2] Kazi hii inatokana na utafiti uliotekelezwa chini ya mwamvuli wa mradi wa utafiti wa Doing the City. Socio-Spatial Navigation in Urban Africa, ulioongozwa na Prof. Dr. Beck, Rose Marie and Prof. Dr. Katja Werthmann (Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani) na kufadhiliwa na Deutsche Forschungsgemeinschaft (DFG), kwanzia mwaka 2017 hadi 2020.

## Upapasi, Mapapasi, Muchi

**Bahati[3]:** Kabla hatujaanza kuchambua upapasi kwa undani, nikuulize kuhusu picha mbili ulizonirushia juzijuzi kwenye Whatsapp ukiniandikia "ofisi yetu imeshauzwa"[4]. Katika picha zote mbili njiapanda inatokeza katikati, upande wa kushoto kuna gari kadhaa ambazo zimeegeshwa ukutani mwa jengo ambalo zamani lilikuwa shule, miaka michache iliyopita likawa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, ila leo hii halina bango lolote linalolipa jina wala madhumuni. Katika picha moja, mtazamo unatokea kivulini mwa mti-kivuli; katika picha nyingine mtazamo unatokea ngazi za kuingia dukani mwa sonara, kando ya benki, kabla ya kupinda kuelekea Forodhani. Aliyepiga picha ndiye wewe Muchi, ukirukaruka kwenye kona hiyo ya mjini, kama kawaida yako katika kila siku yako ya kazi. Imetokea nini kwani? Ulikuwa na maana gani uliposema "ofisi imeuzwa"?

**Muchi:** Nilikuwa na maana kwamba ofisi yetu ambayo tulikuwa nayo hapo zamani, ambayo tukikutana sisi wenyewe, jinsi ambavyo tunajiita mapapasi, tunakaa pale nje na kushirikiana kufanya kazi zetu na leo hii ofisi imeuzwa na itakuwa hatuna mamlaka tena kukaa hapa nje, tutakuwa hatuna mamlaka ya kujitawala kama tulivokuwa tunajitawala zamani. Hata pembezoni mwa duka la Tanzanite, tunajaribu kukaa lakini haipendezi kama tulivyokuwa tunakaa mwanzo katika ofisi yetu, na tunaona uchungu sana kwamba vitu vyetu tunavyovitegemea vinauzwa kwa hoja ya kuwa ni vya serikali. Kwa hiyo, tunasikitika sana sisi na mateksidreva kwamba jengo lile limeuzwa. Tunajitahidi kutafuta ofisi mpya, bado tunaendelea kutafuta ofisi yetu.

**Bahati:** Bila shaka kuuzwa kwa jengo hili ni pigo kubwa sana kwa maisha yenu ya kila siku, tukio dhahiri la mkondo mkali wa kibepari ambao kila kona ya mji mkongwe inasombwa na kuzolewa nao, ukiitikia wito wa serikali wa kuimarisha sekta ya kitalii (Prestholdt 2008). Kwa hivyo ofisi yenu imeshauzwa, ila haijauzwa. Mnamo mwaka 2019, ofisini kulikuwa hakuna duka la sonara. Badala yake kulikuwa na hekaheka za kulikarabati, seremala na vibarua wakiingia na kutoka bila mapumziko, makelele yao na ya vyombo vyao vya kazi yakiongeza ghasia ya kona hiyo, ghasia zikitokana na sauti za gari, wapitanjia, wauza sigara na njugu, ndege, upepo, mawimbi ya bahari.

[3] Nilipokutana na Muchi na mapapasi wenzake mara ya kwanza, nikiwa mwanafunzi wa Kiswahili, ulikuwa mwaka wa 1995. Nilipowasili bandarini Zanzibar pamoja na rafiki yangu wa karibu, ilikuwa mchana na kulikuwa na shamrashamra za kawaida, watu na vitu tele vikikimbiliana na kupishana. Kijana mmoja alitujia akizungumza Kiingereza na kutuuliza ni wapi tunapokwenda na nini tunachotaka kukifanya. Wakati ule hakukuwa na intaneti wala simu za mkononi, nasi hatukuwa na ujuzi wowote kuhusu Unguja wala Zanzibar kwa jumla, yaani giza! Nilimjibu nikizungumza Kiswahili kwa sababu siku zile sikujua kuzungumza Kiingereza isipokuwa zile sentensi mbili tatu nilizokuwa nimefundishwa shuleni, yaani Kizungu hakikuwepo haswa! Bado nakumbuka sura ya kijana huyo, huku akisisimka, kushangaa na kufurahi kwa sababu ya kuzungumza Kiswahili. Hapo ndipo nilipopewa jina la Bahati ninalolibeba na kulitunza kwa furaha mpaka leo. Baadae nimepata kufahamiana na mapapasi wote wa siku zile, na ndipo safari ya urafiki wetu ilipoanza, urafiki uliokua nikishirikiana maisha nao, na familia zao, nikishuhudia raha na changamoto za kazi yao. Urafiki huo umedumu mpaka leo juu ya - na licha ya - mazoea ya kimaisha, matukio ya kisiasa na changamoto chungu nzima. Najisikia fahari kupata fursa hiyo ya kuwa na mapapasi.

[4] 8 Aprili 2022, kama saa 6 mchana hivi.

Na sauti za madereva wa teksi, za watoto wakienda na kurudi shuleni au chuoni, pamoja na sauti za watalii na watembezaji wao, bila shaka sauti maalum ya Muchi, inayoimba kwa sauti ya juu, kila mmoja anaitambua!

Tupo mtaani Shangani, Shangani Posta, wenyeji wanavyopaita, tupo ofisini, wewe Muchi ulivyonambia, ukinielezea vile benchi lililoko kivulini, ukutani mwa duka hilo la sonara, ndo karatasi, nawe mwenyewe ukirukaruka kujitafutia riziki ndiye kalamu. Tutarudia hapo tena baadae kidogo, ila sasa hivi tufafanulie kinachoendelea. Tupo Shangani, mtaa wa Mji wa Zanzibar ambao unasemekana kuwa wa zamani zaidi, kwa vile karne ya 12 ulikuwa kijiji cha wavuvi kilichokua na kukuzwa kuwa kiini cha mji wa baadae, kwa ukaribu wake na bahari, na umuhimu wake kwenye mikondo ya biashara iliyochorwa baharini (Ho and Sheriff 2014, Sheriff 2010, Bissell 2011). Hapo ndipo mnapowakuta watu wazima, waliokuwa vijana miaka ya 80 na 90, wanaojulikana kama mapapasi. Hebu tuelezee papasi maana yake ni nini, ni nani, jina hilo ulilipata vipi? Upapasi ndo nini?

**Muchi:** Papasi ni mdudu mmoja anayehangaika ambaye hana malengo maalum; anaweza kuishi kwenye paka, ng'ombe, mbuzi hata kuku kwa kunyonya damu. Na kunyonya yenyewe ni kwa ajili ya kupata kula yake, sio kwa kumwathiri mtu zaidi, no. Siyo kisawe cha minyoo, kama vile Kenya. Na hata hivo, jina hilo lililokuja kutuselelea sisi, ambalo tukalikubali kuitwa na Mista Mitu miaka ya Themanini, linatokana na vitendo vyetu, kazi yetu na wageni: tunapokutana na wageni tunawapa changamoto fulani, furaha, vichekesho. Hata na wao wanapata ujasiri zaidi kujiamini kwamba mimi nipo na mtu mmoja ambaye anaweza kunisaidia matatizo yangu na kuenjoy holiday yangu. Ndipo hapa tunajaribu kufanya kazi nae ili kupata kula yetu sisi kama anavyokuwa anapata kula yule mdudu anayeitwa papasi, ambaye baada ya kushiba na kudondoka, na sisi baada ya kupata chakula chetu, tunadondoka. Nafikiri wageni wanafurahi mpaka kuhadithia huko kwao nimekutana na mapapasi ambao ni marafiki, watu wazuri, wanakuonyesha ubora. Na hata ukikutana na mtu mwenye uwezo wa chini kidogo, huendi kupata vitu ambavyo haviwezi, yaani unaleta njia mbili za kupata kila anachokitaka. Hiyo ndiyo maana ya upapasi.

**Bahati:** Na nyinyi mapapasi mnamo miaka ya 80 mlikuwa ndio wale vijana ambao waliitikia wito wa serikali kugeuza Zanzibar iwe pahala pa kutalii (kwa maana ya touristic destination). Wakati ule, serikali ilikuwa haijawa tayari, muundo wa sekta hii bado ulikuwa haujaundwa wala kukaa sawa, na nyinyi mlianza kupapasia, yaani mlianza kugusagusa hali ilivyokuwa mkajue wapi pa kujiingiza kati, mkijipatia nafasi maalum kama watembezaji wageni, walinzi wao, wapagazi na wafasiri, kisha mkijiajiri kama vijana wenye maarifa maalum na makubwa, ambao serikali na wageni waliowategemea wakati miundombinu ya utalii bado haijakuwepo. Hata hivyo, kuna masimulizi fulani yanayodai kuwa kupapasia ndiyo 'kuposa usasa' kwa maana ya "courting modernity", yakitafsiri 'usasa', kama kutamani kusafiri Ulaya au Marekani, kutamani mwanamke

wa kizungu, pombe na madawa ya kulevya (de Francisco 2004). Kusisitiza hivyo, masimulizi hayo yanahoji kuwa utalii uliathiri jamii ukiiharibu, na mapapasi ndiyo waliobeba na kueneza madhara hayo. Kuna mshikaji wetu mmojawapo ambaye alikuwa papasi zamani ila leo anajihusisha na asasi za kijamii zinazowahudumia walevi na wateja, aliyekataa masimulizi hayo kabisa:

> Upapasi ni uhuni, upapasi ni bangi, upapasi ni unga, upapasi ni kuharibika, lakini nakuambia kitu kimoja, mimi nimefanya upapasi, yote haya siyo. Kwa sababu mzungu hakukamatii bakora kunywa, mzungu hakukamatii bakora vuta sigara, mzungu they are very respectful, ni hiari ya mtu, […] kwa sababu kuna watu waliokuwa mapapasi walikunywa kwa funny na hawanywi, kuna watu wamekaa upapasini hawajawahi kunywa wala kulewa wala kuvuta, […] kuna watu wamekaa upapasini wamekuwa machizi hospital mental, […] wapo watu, wamedata upapasini, […] hii inategemea behaviour ya mtu, umeshaona? Na vile mtu anavyopokea yale mazingira. Kwa hiyo, kila mtu anapokuja upapasini anakuja na malengo yake, na mtu anapofeli malengo ndo mara nyingi sana anaharibika (J. 2019).[5]

Na kweli mapapasi wengine walisafiri na kuondoka wakibeba mazoea ambayo wanadai yaliwaelimisha kukabiliana na changamoto za maisha, kwa vile walijifunza lugha mbalimbali, kuwa na watu, tamaduni mbalimbali, desturi tofauti tofauti. Kwao upapasi ukawa kama chuo kikuu: "Upapasi umeniwezesha kujiamini – unaweza kuongea na mtu yeyote. Unakutana na watu, kabila tofauti, tamaduni tofauti, na wanazungumza mazungumzo tofauti. Upapasi ulikuwa my first university, wapi? Forodhani garden" (M. S. 2018), nafasi ya kujiamini na vilevile ya kuimarisha imani miongoni mwenu:

> Ilikuwa kazi kama ni ajira kwangu mimi, inaniendeshea napata pesa za kujiendeshea mahitaji yangu ya kawaida na kusaidia pia watu wangu wa karibu, na pia kusaidia ndugu zangu na mambo ya masomo na mambo yao madogo madogo. Ninapata pesa za kumudu vitu hivyo. Umenifaidisha kwa kupata kujua mambo mengi, kwa sababu nakutana na watu tofauti, unazungumza mambo tofauti, unapata kujua mambo mengi ulimwenguni kupitia hao wazungu kuzungumza nao, kufanya urafiki, nimepata marafiki wengi kutoka nchi mbalimbali, ambao wengi wanakuja, wanaondoka na kuja tena (A. 2019).

Je, kwako upapasi ukawa nini? Yaani ulitamani kusafiri, kuondokea kwenu, kuwa na maisha nje ya Zanzibar? Ulikuwa na malengo gani, na ndoto gani?

**Muchi:** Kwa kweli upapasi kitu kimoja au changamoto ambayo inakuletea furaha katika maisha yako. Mimi mmojawapo wa mapapasi ambae sikutaka kusafiri wala kwenda sehemu nyingine yoyote, ila upapasi nimeupenda sana kukutana na changamoto za watu, aina mbalimbali. Napata kujua lugha nyingi na vilevile kupata mahitaji yangu ambayo yanaweza kunisaidia mimi, wazee wangu na watoto wangu. Japo hali moja ya dunia ya kimaskini ambayo wazazi wangu ilikuwa yao,

[5] Nukuu nyingi zinatokea mahojano na mapapasi mbalimbali. Wenyewe wameomba majina yao yasitajwe. Kwa hivyo, mtakapokuta nukuu zinazorejelewa kupitia herufi ya (au za) kwanza tu ya majina yao, ya kweli au ya kimaarufu, mtajua kwamba hayo ndiyo mawazo na maoni ya mapapasi.

upapasi ulinisaidia sana, nimewasaidia wazee wangu, nilifanya changambinu nyingi sana, na nikawa tajiri kiasi ili nisaidie wazazi, watoto na familia kwa jumla. Upapasi kwa maana ya kuchukuliwa na wazungu kwenda kuishi katika nchi mbalimbali no, miye nasema yale ni mapenzi ya mtu ambaye aliweka mpango wa kukaa na mtu, na kuzaa nae, na sidhani kwamba mtu akishazaa anataka kukaa mbali na watoto. So, baadhi ya mapapasi walisafiri kupata wepesi wa kimaisha, kusaidia family zao. Upapasi kwa mapapasi ni nafasi ya kusaidia familia zao, wapate mahitaji yao. Na hivyo, upapasi ni kazi bora zaidi, kutokana na kupata pesa kirahisi na unapata rafiki kutoka nchi za nje, kama vile Italy, umeshaona? Kwa hiyvo nimekichukua kama kitu kizuri sana katika maisha yangu, na kweli kimeniwezesha mafanikio, kimeniunganisha na marafiki, kimenipa uwezo wa kuwasaidia wazazi wangu, kimenipa pesa za kuwalea watoto wangu na nilipopata watoto nilisikia furaha lakini. Kwa hivyo, upapasi ni kitu bora zaidi kwangu mimi.

**Bahati:** Kwa nyinyi mliobaki Zanzibar wakati wa mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii, kazi ya upapasi kwa njia fulani ikawa ngumu. Wacha nieleze zaidi. Mwenyewe nakumbuka mnamo miaka ya 90, pale ambapo nimewakuta tayari mko na kampuni zenu za kipapasi, mkifanya kazi kwa kushirikiana magari ya kwenda shamba, mkiwa na mfumo wa kazi ambao mliubuni nyinyi wenyewe, pale ambapo serikali ilikuwa haijajipanga kisekta, pale ambapo serikali ilikuwa inakutegemeeni. Nae papasi mwenzako mmojawapo aliwahi kuniambia:

> Zamani kulikuwa hakuna tour guide na wizara ya serikali walikuwa wanatuhitaji sisi. Wakishindwa jambo wanatuita sisi, kwa sababu sisi tulikuwa tunaweza kumfahamisha mtu, sio kugombana nae. Sisi tulikuwa na uwezo wa kumtuliza mgeni kwa sababu tulikuwa na tricks za kuongea. Kwa mfano siku nyingine mgeni, hata alikuwa ameshalipa lakini angekubali kuja na sisi na kutoa hela tena (M. S. 2018).

Hebu tuhadithie zaidi kuhusu wakati ule wa miaka ya Tisini.

**Muchi:** Unajua zamani Zanzibar ilikuwa kila kitu wanahisi kwamba ni kitu kinyume, zaidi kufanya kazi na wazungu kutokana na dini yetu jinsi ilivyo. Watu walikuwa wanachukulia kama wazungu ni wahuni, wazungu wakikuchukua utaoana nao utabadilisha dini. Sasa ndo maana watu wengi hawakuweka mbele upapasi. Baada ya kuona changamato ya wale wanaofanya upapasi, vipi wanavyotajirika, vipi maisha yao yanavyokua, hata serikali nayo ilijaribu kuunda muundombinu, na kila mtu alijaribu kuona na macho kwamba kumbe wazungu wanaleta changamoto ambazo zinawezesha kupata pesa ya kimaisha. Hata Forodhani tulipokuwa tunapita na wale wazungu, wazee na vijana walikuwa wanatusemea kwenye madirisha, wanatuambia: “Hao, waangalie wao wanatumwa na wazungu, Hao wanani, hao wanani…”, kwa sababu hawajajua changamoto, lakini hao hao sasa hivi wanawamiminikia wazungu, wanataka waoane na wazungu, hao hao wanataka kwenda Ulaya na wazungu. Hapo sasa, wakati serikali iligundua kwamba kumbe upapasi una faida, ilianza kujipanga ili ipate kuudhibiti. Ila upapasi haudhibitiwi, ukijaribu kuufupisha upewe lebo moja, ukiuzuia kwenye mipaka ya tourguiding, basi sio upapasi tena. Sasa, watu wengi walizidi

kujiingiza kwenye kazi za utalii, na sasa hivi kutokana na vile sekta ilivyoendelezwa kupitia tour mbalimbali, basi kazi kwa sisi imepungua kiasi kikubwa sana. Tour zinachukua watu kutoka Tanganyika, Bagamoyo, booking kutoka Ulaya, magari yameshapangika na mfumo wetu wa car-sharing ulibomoka, bei zikashushwa chini kabisa makampuni yetu yakijaribu kudumu, mpaka yamezidiwa na kuvunjwa. Kazi imekuwa ngumu vijana wamekuwa wengi. Kila mmoja hana kazi, anajifanya papasi, anasema twende beach tukafanye kazi. Kazi zimezidi kuwa ngumu zaidi, kwa hiyo Kamisheni ya Utalii[6] wemeunda mbinu mpya, wanachukuwa vikosi vya maaskari, askari wote, magereza, JKU, wanajeshi, polisi wamejaribu kuunda community moja kuwakamata "mapapasi", yaani yeyote anayekutwa barabarani akijishughulisha na wazungu kwa njia yoyote, kwao ndiye papasi. Kwa hiyo, kazi imekuwa ngumu kupindukia, ina changamoto ya uadui, uadui umekuwa mkubwa, kazi imekuwa ndogo.

## Uwenyeji wa Mapapasi

**Bahati:** Ila uhusiano na askari, yaani uhusiano na serikali, haujawahi kuwa na usalama, kuwa uhusiano wa moja kwa moja. Mwenyewe nakumbuka mabishano bila ya mwisho kila mlipokuwa mnasimamishwa vituoni barabarani, kwa vile mlivyokuwa mnashirikiana na wageni, na kwa vile mlivyokuwa mnaonekana. Alivyonihadithia mshikaji wetu papasi mwenzako kuhusu uhusiano na maaskari:

> Haijawahi kuwa easy […]. Labda sasa hivi imezidi kuwa tough zaidi. Kipindi kile ok ilikuwa tough lakini ulikuwa unakwenda kuchukua permit ile ok unaenda shamba kipindi mpaka uwe na ID, unaweza ukawa na ID unaenda zako shamba. Tayari mimi nimo nina ID na kuna mtu mwingine yumo hana ID yule, polisi wanakusimamisha: mbona mmechanganya? Hii ilikuwa inaniumiza sana. Kwa nini mmechanganya Wazungu na Waswahili, why not? Si kuna mtu ndani tayari ana ID? Saa nyingine unachukua mtu pengine ni Mmarekani au sijui mgeni, ni mweusi anakuja askari anataka kumshusha: shuka wewe papasi. Hiyo ilikuwa inaniumiza sana. Lakini wao ndo hawajui, umeshafahamu? […] Wanatafuta sababu tu wapate. Kwa sababu mpaka wageni wamekubali kuwa na mimi kwenye gari nafanya nao trip, ujue wako salama, wameshanikubali, kwenda usiku labda mkatafute sehemu mkakaa mkalinda hiyo sehemu afadhali, lakini wageni niko nao (O. M. 2019).

Wewe mwenyewe unaonaje uhusiano wenu na askari, jana na leo?

**Muchi:** Uhusiano umekuwa mgumu zaidi kwa sababu zamani tulikuwa tunapita vituoni tunasimamishwa, tunapata changamoto, lakini mwishowe wale watu wa vituoni walijenga urafiki na sisi kwamba hawakuwa na matatizo, wanashirikiana na serikali, lakini wanakuja kutuambia. Lakini changamoto za sasa hivi zimekuwa ni nzito kwa sababu hivi vikosi ambao wamchukua mtu magereza ambapo wameshawapeleka wafungwa, ukiwaleta mjini amshughulikie papasi

[6] Kamisheni ya Utalii iliyoanzishwa mwaka 2009 ni taasisi inayojitegema na iliyopo chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

watamshughulikia papasi kama mfungwa. Kwa hiyo, ataleta uadui zaidi kwa yule papasi. Kwa hiyo, imekuwa ngumu, wanakukamata, wanakuuliza kitambulisho, mbele ya wageni, hawakupi nafasi kusema “ah bora nikuachie, halafu nije baadae nikukamate”, anakukamata, anakutia pingu mbele ya wageni, analeta picha mbovu mbele ya wageni. Halafu hajaweza kuwaelimisha wale wageni kwamba “bwana, fulanifulani, anatakiwa yule mtu awe hivi hivi hivi hivi”. No anakuja: “kitambulisho kiko wapi?” “Mbona sina!?” Kwa hiyo, ukifika wewe anakwenda kukukamata, kukutia pingu, anakukamata kama mtu ambaye anauza madawa, au umewahi kuiba kuonekana unatafutwa. Miye nilikuwa naomba serikali yetu kidogo labda ipunguze ile kuweka watu vikundi kama vya askari, waache wale watu chini ya Kamisheni ya Utalii wamalizie wao wenyewe. Nafikiri ndo hiyo changamoto yenyewe mojawapo. Ndiyo maana hata unakuta mapapasi wengi wanajaribu kuleta maendeleo, lakini wanarejeshwa maisha nyuma. Vipi? Kutokana mtu ana family, ana watoto wanakutegemea kimaisha. Hawaoni vile wanavyotengeneza akili za kiadui zaidi, lakini serikali wasiangalie watu ambao wanataka kuboreka kama maadui.

**Bahati:** Inasikitisha kukusikia ukitamka uadui, pale ambapo upapasi msingi wake ulikuwa imani, mshikamano, urafiki, hata kama kulikuwa na mashindano, mshindi yule anayemfikia mgeni mapema zaidi na ‘kumwibia’ mwenzake, mwisho wa siku, kipato kilikuwa mkusanyiko wa kila mmojawenu mkigawa hela sawasawa. Nilipata kuelewa kuwa mateso kutoka kwa maaskari yalikuwa ya aina mbalimbali kuanzia kuaibisha hadi kupiga, ya kisaikolojia na ya kimwili vilevile. Mlivyonihadithia, mara nyingi sana tatizo lilikuwa linaanzia swala la kitambulisho, kibali yaani. Mwisho wa miaka ya 90 serikali iliamua kurasimisha kazi zote zilizohusiana na utalii, wakaingiza sharti la kuwa na kibali. Wewe kibali ulikuwa nacho? Na leo je, unacho?

**Muchi:** Kibali mimi sasa hivi ninacho, ila vibali vya zamani na cha sasa hivi tofauti, kwa sababu kile cha zamani kilikuwa permit ya Trust Moja Government, na unaweza kufanya kazi zako. Lakini sasa hivi imekuwa changamoto ngumu zaidi kutokana na wale maaskari ambao wanaruhusiwa kuwaangalia, kuwakagua watu ambao hawana kibali; wakimkuta mtu ambaye ana karatasi, amepewa risiti kwamba kibali chake kitakuwa tayari mwezi ujao, still wanamzuia asiweze kuwatembeza wazungu, asiweze kufanya hivi, na hivi na hivi…sasa, hata kama huna kibali inatakiwa mtu ajaribu kumpa onyo, ujaribu kumwelewesha zaidi, ujenge urafiki vya kumwambia ajielewe apate kujua kesho yake nini afanye. Lakini kumwambia mtu by force, kwamba “lazima kibali, lazima kibali”, ah-ah, miye nafikiri serikali ilete suluhisho tofauti kuhusu hichi kibali.

**Bahati:** Nahisi swala hili la kibali tulifafanue zaidi. Maana yake halihusu kibali chenyewe tu, bali mtangamano baina ya askari na nyinyi, uhusiano ambao wenyewe umebadilika tukilinganisha leo na jana. Tangu mwanzo wake, kibali kilikuwa kinasema kwamba uliruhusiwa kuwa tour guide, lakini wewe pamoja na washikaji wengine mlivyonihadithia kazi yenu ya upapasi, sio ya tour guide peke yake, kwa hiyo kibali hakifai. Walipoingiza kibali, ndipo hali ya kazi ya upapasi ilipopakwa

“rangi” nyingine, ikitafsiriwa kwenye lugha ya kisheria kupitia vivumishi kama vile halali, rasmi, au hali kama uhalifu, na uhuni, mpaka ikawachukua mapapasi kama mfanyakazi mmoja wa Kamisheni ya Utalii alivyoniambia: “Watu wa ungaunga tu wale, wanaokera wageni. […] wao hawaaminiki. […] watu wanaovuta ungaunga lazima wafuge zile nywele zile, dreadlocks sijui, halafu zamani walikuwa wanakatwa, sasa mtu aliye na kile kibali kile anajua zile hatakiwi kuwa nazo”[7], akisisitiza uwezo wa kibali chenyewe wa kuwapa wanaojishughulisha na wageni uhuru na ruhusa ya kukalia na kuwepo mjini kwa njia maalum. Nae papasi mwenzako anaitikia hapo:

> Papasi ni mjasiriamali, ndiye papasi, mtu ambaye anapigana kujipatia maisha mapya kwa njia zilizo na usumbufu, mbali na tour guide ambaye kasomeshwa. Papasi hakupita skuli lakini anaelewa, anafahamu, anahitaji kupatiwa heshima kama binadamu wa kawaida. Lakini kwa serikali papasi ni mteja, wakati sisi tulitengeneza trust baina yetu sisi na watalii (A. R. A. 2019).

**Muchi**: Tofauti na mtu ambaye ameajiriwa, kwa sababu ana nia kubwa zaidi kutokana na yupo kwa ajili ya wazungu kila wakati, hasubiri mpaka aitwe, ajaribu kujipendekeza yeye mwenyewe, anajaribu kutafuta changamoto, kuhisi vipi mgeni anikubali, kwa sababu papasi na tour guide kitu tofauti. Tour guide ni mtu mmoja ambaye anatakiwa…anatengewa tayari, ni kama mtoto na mama, kwamba unampikia chakula mtoto, ale, atoke, acheze. Tour guide anaambiwa atachukua wageni kumi awazungushe mjini mpaka saa fulani, halafu awarudishe. Lakini papasi ni mtu ambaye anafight mwenyewe, anajipeleka mwenyewe, anajiunganishia urafiki yeye mwenyewe, anajaribu kuzunguka na mtu, hajui muda gani atamaliza kuzunguka nae. Kama ikiwa mpaka kesho atazunguka nae mpaka kesho, kama ikiwa mpaka saa ngapi… ni mtu ambaye akajipa free mwenyewe, kwa kutengeneza huo uhusiano, urafiki wa kazi… Miye naona papasi ni mtu muhimu sana, tofauti na tour guide, kwa sababu papasi ni mtu ambaye anaweza kukuhadithia bila kuulizwa kitu kinachokupa interest wewe mwenyewe, na anaweza kukuhadithia kitu ambacho hukutegemea kwamba utafafanuliwa hichi kitu, lakini tour guide vitu vingi sana wanafeli kutokana na kuonesha sehemu muhimu kama hawajajua watu. Atampeleka Freddy Mercury atampeleka Slave Market, atampeleka Market, lakini hakupi wewe mjini vipi jinsi ulivyo, yule nani, yule hivi, watu wanaishi hivi, lakini naona papasi ni bora zaidi kwa sababu mpaka anakutafutia njia ile mwisho atakuona wewe kwa urafiki zaidi. Papasi atakupeleka mpaka kwao kula ugali, lakini tour guide hatakupeleka kwenu ukale ugali. Papasi atakuendesha shamba hujawahi kuona, tour guide hawezi kukuonesha “huyu ni mbu, atakuletea malaria”, lakini papasi anakuonesha. Lakini tour guide atakuambia “ah ni mbu tu”, hakuambii ukweli wenyewe, kwa hivyo papasi ni yule mtu ambaye anatoa ukweli kutoka moyoni kwa changamoto zaidi. Au unaonaje?

**Bahati:** Nakusikiliza, nahisi kwamba kuwepo au kutokuwepo kwa kibali kuna maana na athari nyingi mbalimbali, kunasababisha ukweli ulioongelea hapo juu usiwe mmoja, bali uguswe kwenye

[7] Mahojano yaliyotkoea tarehe 20 Februari 2019 ofisini mwa Kamisheni ya Utalii (Zanzibar mjini, mtaa wa Amani).

uwingi wake. Papasi mwenzetu alivyosisitiza, “serikali ingekuwa ingetuunga mkono kwa sababu tulikuwa tanafahamu, tulikuwa na umoja watu kama 40 au 50 tulikuwa tunatengeneza mambo mengi. Baadae serikali walianzisha ZATI *[yaani Zanzibar Association of Tourism Investors]* na wamesahau community tuliyokuwa tumeitengeneza sisi” (A. R. A. 2019). Ni dhahiri vile kibali kikawa kikwazo kinachotiliwa mkazo mpaka kifiche historia tofautitofauti za utalii, historia ya upapasi ndiyo mojawapo: na ndicho hicho kibali kinachobeba na kuunda uchungu kwa vile wengi wenu wamejihisi wanapingwa, wanadharauliwa, hawana nafasi mjini Zanzibar.

## Siku Moja Ofisini – Nafasi ya Upapasi Mjini Zanzibar

**Bahati:** Haya, turudi ofisini utuelezee siku yako mojawapo ya kazi, unapoamka asubuhi mpaka unaporudi nyumbani ukalala.

**Muchi:** Mimi asubuhi nikiamka naamka saa mbili na nusu, wakati zamani nilikuwa naamka saa kumi na mbili na nusu kutokana na upapasi wa zamani ulikuwa na changamoto kubwa ya alfajiri: kwamba ninaamka, natoka zangu mtaani, napitia hoteli baada ya hoteli kuangalia kama kuna wageni wanaotaka kwenda shamba au kisiwani au wanataka kufanya chochote kile, ila changamoto za kazi zilikuwa za asubuhi. Kwa hiyo, nilikuwa nafika Malindi asubuhi, kutoka Malindi napanda gari ya sharing napitia hoteli. Nikitoka Malindi napita Flamingo, nikitoka Flamingo, napita Kiponda, nikitoka Kiponda ninaishia Manchi Loji[8]. Gari tayari, tulikuwa tunaenda shamba wakaenjoy tukazidi urafiki. Ila sasa hivi naamka saa mbili kamili, nakoga, nikimaliza kukoga nakwenda zangu ofisini, njia ya Posta na Jumba la Ardhi, nikifika pale, nakaa kwenye benchi. Nakaa na wenzangu pale, tunajaribu kuleta changamoto ya siku ya leo. Tunafika kuambiazana kama wageni jana wameingia wengi, leo kidogo, kwa hivyo, tukifika pale tunaanza kutega wageni, wanaotokea juu kuja chini, wanaotokea chini kupanda juu[9]. Tunajaribu kuwauliza nini wanataka kufanya kupanga kazi zote za leo. Changamoto inaweza kuwa vilevile mgeni anavyoamka, pengine hajaamka vizuri analeta zake, au ameamka vizuri, lakini hana plani yoyote, akakuuliza wewe nini cha kufanya, na atakuamini vile unavyopanga akaenjoy, au ananipangia mwenyewe vipi nifanye. Tunaweza kwenda kisiwani asubuhi, ukirudi kama hujachoka ntakupeleka spice tour, na kama unataka baadae twende zetu shamba ukakae one night, na utakaporudi nitakuja kukuchukua nikupeleke East. Halafu tunapanga itakuwa kiasi gani. Mara mgeni anakulipa kazi zako zote, mara leo hivi, kesho hivi: sawa! Jinsi upendo anaonionyesha mgeni. Labda anahitaji company yangu, sawa! Kwa hivo kuwepo ofisini maana yake kufanya kazi ndefu zaidi. Unaenda kule unajaribu

[8] Kona ya Shangani Posta ni maskani pekee iliyobakizwa miongoni mwa maskani za mapapasi nyingi zilizokuwepo mji mkongwe kama nafasi zao wenyewe, pahala ambapo walikuwa hukutana mnamo miaka ya Tisini – Malindi Guest House, Falmingo, Manchi na Warere (zote hizo hoteli ndogondogo), Forodhani, Shangani Posta, Culture Musical Club na Africa House.

[9] Kutokea chini, maanake kutokea upande wa Forodhani au Kileleni. Kutokea juu maanake kutokea Vuga, Shangani Posta.

kuweka hiyo smile unajua? Ndo maana nikakuambia tour guide na papasi ni vitu viwili tofauti. Na kitu kikubwa cha kwanza ni smile. Papasi ana smile kubwa zaidi kuliko guide, ya kutosha yaani, mpaka mgeni ajihisi kwamba anataka kuwa na wewe. Kwa sababu wenzetu maisha wanayoishi tofauti, Ulaya hakuna ujirani na ukaribu kama wa kwetu, lakini wakija huku wanakuta urafiki, ukaribu zaidi. Kama wana watoto, unajituma zaidi mpaka na mtoto awe rafiki yako. Hatima yake unakuta umejenga urafiki na mwisho wa siku mgeni akikuuliza nikulipe kiasi gani, unamwambia “uangalie uwezo wako wewe mwenyewe” nae anajipa moyo akulipe wewe zaidi. Ile kupinga vile watu wengi wanavyofikiria kuwa “kumbe wao (mapapasi) wanataka pesa nyingi”, lakini hawajui kwamba ni akili na nguvu zinakufanya upate pesa zaidi: kujiuliza kwa mfano kwa nini mgeni amenikataa, au ni vipi nishinde imani yake? Na akili hiyo inatumika ujenge urafiki, ujenge uhusiano ulio na imani ndani yake. Utaniona nakutana na mgeni yuleyule mara tatu kwa siku: mara ya kwanza kanikataa, mara ya pili kanikataa, najaribu kuzungumza nae, mpaka akajenga urafiki. Lakini watu wengi wanaleta jealousy hii kwa kumwita papasi yule mtu asiye papasi, kwa sababu utumizi wa papasi tofauti na utumizi wa mtu yule anayefanya kazi serikalini. Kwa nini? Kwa sababu papasi anaweka urafiki kwa ajili ya kesho, sio kwa ajili ya mshahara wa mwisho wa mwezi! Kwa hiyo utumizi, jitihada za kazi yaani, tofauti. Hata hivyo, papasi anaonekana kama yule anayepata pesa nyingi, na hayo yanaleta uadui zaidi.

Kwa hiyo, kawaida naendelea na kazi mpaka saa moja usiku, ila nikiwa na rafiki ambaye anataka kutumia muda mwingi zaidi, najaribu kutumia muda mwingi zaidi, atakaposema yeye akachoka na mimi ndio nimechoka, na kama ni kuendelea tunaendelea. Matumaini makubwa mimi upapasi ni kujenga urafiki mwingi na watu wa nje ya nchi yetu, na watu ambao wana upendo ukaribu, ambae tutaweza kusaidiana katika maisha. Nashukuru kwa hilo, upapasi umeniletea mengi katika maisha yangu, ninayoishi na mke wangu watoto wangu, familia yangu. Upapasi ni good time for me.

**Bahati:** Sawasawa. Lakini siku hizi mara nyingi tunapokuwa tumekaa kwenye benchi siku nzima, mwisho wa siku ‘tumeupa msokoni’[10], si ndiyo. Na hayo ndiyo mabadiliko ya maisha, majukumu pamoja na hali ya kiuchumi, yaani vile kazi ya kupapasia tukilinganisha miaka ya 90 na leo hii, tofauti. Mshikaji mmoja aliyekuwa papasi zamani, na sasa hivi ana tour operator, alinielezea tofauti baina ya upapasi wa zamani na wa leo:

> Upapasi kipindi kile tumepata pesa, tumejenga nyumba Alhamdullilahi, tumepata income kubwa, tumepata kusafiri nchi tofauti tofauti, kwenda kuangalia maisha, kwa hivo nikarudi nyumbani hapa, nimepata kuoa, naishi na familia vizuri, nawasomesha watoto. Sasa hivi, tofauti na kipindi kile upapasi, tuliona bora tubadilike, tuweke tour operator, tulihisi kwamba lazima tubadilike, tumekuwa wakubwa haiwezekani kwamba kila siku tuwe papasi twende mbio huku na huko […]. So tunaona sasa hivi

[10] Mchezo wa huko kwetu Ng’ambo, mchezo wa gololi. Maanake ni kwamba leo tangu asubuhi tumesimama ila hamna kitu!

> tumeshakuwa wakubwa tubadilike, tuanze tutulie kuliko kwenda mabio tu, tulikuwa tunaenda mabio tu sisi, [...] pesa tunapata, tunatumia sana, kwa starehe, ndo ujana (S. A. 2019).

Nawe ulivosema, zamani kulikuwa na maskani nyingi, na kazi ilikuwa tofauti, ila leo, mmebakizwa na ofisi moja tu, Shangani Posta nanyi mnabaki ofisini: vyovyote vile, msimu wowote ule wa high-season au low-season, hakika nitawakuta ofisini. Zamani kulikuwa hakuna kusubiri sana, kila kitendo chenu kilitekelezwa mbioni. Kulikuwa na mwendo maalum wenye kasi fulani, mzunguko wa pekee kupitia maskani zote za mapapasi. Ila leo upapasi unaanzia ofisini…

> *Ofisini kuna benchi. Liko kivulini, karibu na duka la sonara. Muchi na mimi tumekaa tukipiga gumzo. Mbele yetu kuna barabara inayopitia Kileleni na Hayati, leo eneo la hoteli zenye nyota nyingi tu. Barabara inafikia konani, inapounda njiapanda pamoja na ile inayotokea mahakamani kupitia Posta na kuelekea Forodhani. Njia zote hizo zinamimina wageni ofisini. Mkono wake wa kushoto kulikuwa na shule zamani, baadae ubalozi wa Marekani, kisha jengo likawa nyumba ya Wizara ya Ardhi, na leo, leo limeuzwa, jengo lake likitaka kulisha sekta ya utalii zaidi na ziada. Natizama upande wangu wa kulia, ghafla naona bahari, kwa mbali kidogo. Pwani kumejaa, kuna hekaheka za wenyeboti wanaotafuta riziki zao. Upande wa kushoto kuna Livingstone, kilabu kilichorithia jina lake "mpelelezi" maarufu aliyewahi kuishi hapo katika karne ya 19. Leo kilabu kinamilikiwa na mjukuu wa Mh. Abeid Amani Karume, rais wa kwanza wa Zanzibar. Jengo limetandika jukwaa (scaffolding); litakuwa hoteli mpya hivi karibuni, labda leo hii iko tayari. Turubai la rangi ya machungwa limeraruka: upepo ukivuma linachacharika likitoa sauti yake maalum. Tumejaa vumbi lake. Upande wa kulia kuna mgahawa na diving center. Zamani, kulikuwa na ubalozi wa Ujerumani.*
>
> *Muda unapita. Tunasogeza benchi. Benchi linasogezwa na kusogea likifuata kivuli, ila lipo likiendekeza mwenendo wa watalii kufuatana na mahadhi ya mji. Au ni mji unaofuata mahadhi ya watalii? Tunasogea pamoja na benchi. Kivuli kinafifia mpaka kutoweka kikishindwa na miali ya jua kali la mchana. Wageni wamejificha hotelini. Adhana inasikika kwa sauti kubwa; ghafla kila mmoja anatoweka ofisini akielekea msikitini. Muuza ice-cream nae anaondoka akimkabidhi biashara yake yeyote yule anayejitolea; madereva wa teksi wanaondoka kwa zamu. Kwenye benchi hakuna mtu. Muchi amesimama. Shuwari; hakuna mtu. Ila watu wapo, mwenendo unaendelea ukifuata mahadhi tofauti. Naye Muchi haondoki. Anasubiri.*[11]

Kuna uzuri gani kwenye kukaa kwenye benchi kwa masaa, mkisubiri? Kwani mnasubiri nini?

**Muchi:** Uzuri kukaa maana yake kuna changamoto nyingi sana. Mojawapo, kuna hadithi mbalimbali, unakutana na watu tofauti: madereva wa teksi, ambao tunarushiana maneno yetu, yanapambana kidogo na yakipambana yanaleta urafiki zaidi. Kuna watu wazima, vijana, watoto wakipita harakati za kwenda. Ila kubwa zaidi ambayo imetuweka kwenye lile benchi ni kwamba tunafurahia vipi maisha ya leo tutaishi. Jinsi gani tutaishi sisi, watoto na wazazi. Na hata kama wewe umeupa msokoni, jirani atasema, "hujaupa hivo; mimi kidogo nimedondoadondoa, kamata

[11] Picha ya kona jinsi ninavyoichora fikrani mwangu kutokana na kumbukumbu zangu.

ile leo hii”. Tunapata kunywa maji zaidi, kwa hiyvo kuna imani fulani, huruma ya upapasi ya kusaidiana wenyewe kwa wenyewe. Hatupotezi muda, tukikaa kwenye benchi, tunatengeneza kazi ya kesho. Na tumesikitika kwamba ofisi yetu imeondolewa katika ukurasa wa kuvutia zaidi, kwamba wageni hapo wamekaa chini ya miguu yetu. Tunajaribu kukaa kwenye ngazi ya duka lile. Kwa hiyo, ile ofisi kubwa yenye air condition imeuzwa, tupo ofisi ndogo, lakini kazi zinakwenda. Tunapata changamoto huku na huko, upepo kutoka pwani. Hata kibaraza cha diving, nacho pia tumeondoshwa, tunakaa kwa pembeni huko. Lakini ni sawa, sio mbaya. Changamoto zikizidi, nasi tunazidi kutafakari.

**Bahati:** Kwa hiyo kusubiri hapo ni kitendo kisichofuata utaratibu wa mwendo wa saa, siku wala miaka, bali ni kitendo kinachotokea nafasi hiyo hiyo ya kukaa kwenye benchi, ikichuja wakati uliopita, wakati uliopo ambao umejaa mazoea ya miaka zaidi ya 20 kwenye kazi hiyo, na vilevile ikitarajia siku za usoni, zisizo na uhakika wowote (wa kupata riziki, kwa mfano, wa kufanikiwa). Kusubiri ni nafasi inayokuhimiza na matumaini, mategemeo, uwezekano na uwezo. Nafasi inaweza kutokea wakati wowote, inataegemea bahati na Mwenyezi Mungu: “God amenipa kitu ambacho nakibeba; pengine kwenye ofisi isingekuwa hivi, nisingejua mambo mengi. Nimepata kujua mambo mengi sana ambayo watu wanateseka nayo. Nimebahatika. I am so proud, I am so proud. Na ndo maana mpaka sasa hivi ni papasi, si kitu ambacho nakifikiria kwamba ni shame” (O. M. 2019). Vilevile, mwanasosholojia Susann Ludwig akichambua dhana ya ‘*la chance’* miongoni mwa vijana ambao ni wahitimu wa shahada ya kwanza mjini Bamako, anabainisha kwamba ni matokeo ya muunganiko wa masharti na vitendo vya kuitafuta nafasi hiyo. Hii ina maana kwamba ni sharti mtu aitambue bahati (yake) kadiri inavyojitokeza au anavyopewa na Mungu, aitafute na kuitumia: “*la chance* is the result of a combination of prerequisites and practices of looking for *la chance*” (Ludwig 2017: 80); kisha lazima aende nayo: “[…] university graduates in Bamako create certainty as they open up *la chance*. It is their convictin that *la chance* exists, which is informed by their experience, in combination with their practices of ›opening up *la chance*‹ (that is looking for *la chance*, finding *la chance*, and working with *la chance*) that create certainty” (*ibid*.: 88). Kwa hiyo, nafasi yenyewe inaundwa kwenye uhusiano baina ya mtu na hali iliyopo wakati maalaum na pahala maalum. Hivyo, kukaa kwenye benchi na kusubiri ni vitendo vinavyobeba fursa nyingi, na vinavyokuwezesha kuendelea, na kutokukata tamaa: “a goal oriented meaningful practice” (Masquelier 2013: 472). Vitendo hivyo huzalisha thamani kwa kuhuisha biashara mahala pa kazi, kuwezesha uchumi wa kibiashara na ukarimu “produces value, both by activating the commercial potential of the site and by facilitating economies of exchange and generosity” (Basil and Bize 2018: 82)[12]. Ndipo mshikamano na imani ya kipapasi inavyorejewa

[12] Kazi hizo mbili zinahusu vitendo na maeneo mawili tofauti. Mwanaanthropolojia Adeline Masquelier alichambua maisha ya vijana na tabia ya kutengeneza chai na kukaa sana kivyao nchini Niger; matokeo ya utafiti wake yanaonyesha jinsi tabia ‘ya kawaida’ inavyochukuliwa kama ‚kutofanya lolote‘ pale ambapo hakuna ufahamu wa muktadha na uhusiano unaozalisha kitendo chenyewe. Ibrahim Basil na Amiel Bize ni wasomi waliochambua kazi

pamoja na lugha yake. Ndivyo hivyo, nafasi inaweza kutokea wakati wowote ofisini, lakini, mshikaji wetu Shebi alivyotuelimisha, nafasi inatokea mtu nafsi yake. Na ndiyo benchi lile lililopo ofisini sio sitiari tu ya nafasi ya upapasi, sio dalili tu la kusubiri-kwa-ajili-ya-kupumzika wala la kusubiri-fursa tu, bali linalozalisha nafasi pamoja ya nafsi za mapapasi: kwa maneno tofauti, hakuna nafasi yoyote inayowezekana isipokuwa kutokana na kuhusiana, kugusana na kutangamana kwa mapapasi, ujanja na mazoea yao, na benchi, madereva, wazee, vijana, maneno yao, kona, duka, magari n.k.. Ni kutokana na uhusiano huo kuwa nafasi ya upapasi, ambayo siyo nafasi yoyote, inazalishwa.

## Kuelekea Hitimisho – kutoka (Hi)Stori(a) hadi Historia

> *It matters what matters we use to think other matters with; it matters what stories we tell to tell other stories with; it matters what knots knot knots, what thoughts think thoughts, what descriptions describe descriptions, what ties tie ties. It matters what stories make worlds, what worlds make stories* (Haraway 2016: 12).
>
> *Kila hadithi ya maisha inapaswa kusimuliwa* (Ghassani 2021).[13]

**Muchi na Bahati:** Licha ya kwamba tunawaunga mkono mwanafalsafa, mwanabiolojia na mwanafeministi Donna Haraway na mwanahabari na mshairi Mohammed Khelef Ghassani wakisema kwamba kila hadithi inamata (ina mashiko), inapaswa kuhadithiwa na ina umuhimu wake, sababu zetu za kutaka (hi)stori(a) ya akina mapapasi isimuliwe ndiyo kufafanua historia yao na ya mjini iliyo tofauti na ile inayoundwa na masimulizi ya tawala ya kitaifa na kimataifa, pale ambapo serikali ndiyo taasisi iliyokataa kuhalalisha na kurasimisha kazi yao ilivyo, yaani kazi ya upapasi. Kwa ajili ya kuhitimisha tutarudia yale tunayoona muhimu ili tuelewe kuwa kitendo cha upapasi ni kitendo kinachotokana na uhusiano baina ya mapapasi na mji, mwendo na mwenendo wao, pamoja na masimulizi kuhusu wao. Kwanza kabisa, historia hiyo inatokea Ng'ambo. Tunavyojua hadithi na historia zihusuzo Zanzibar mjini, kawaida mtazamo wao ndo mtazamo wa Mji Mkongwe, au vile ulivyokuja kuitwa "Stone Town", mawe yakipakwa utambulisho maalum, aina ya uwenyeji pekee (Bissell 2005). Basi kawaida mji wa mawe hutazama Ng'ambo 'kwa mbali' ukibuni na kuunda 'kinyume chake', yaani 'ng'ambo yake'. Lakini leo historia yetu ina mtazamo wa 'watoto wa Ng'ambo', vijana wa kizazi cha pili cha mapapasi, ambao Muchi ndiye mmojawapo. Historia hiyo inatuelimisha juu ya maisha ya vijana ambao hawakuwahi kutambuliwa kwa njia yoyote ile isipokuwa wahuni, mabeachboys, watu wa ungaunga, wanaotamani 'usasa' maalum. Hata pale wanapochukuliwa kama mseto (wa kijamii) – na nadhani sote tunakubaliana

ya madereva wa bodaboda mjini Nairobi, wakidhihirhsa dhana ya ‚shimo' kuelewa umuhimu wa nyakati ambapo wahusika hawana kazi bali wanaonekana wanasubiri tu kupata abiria. Kazi zote mbili zinavutia sana kwa sababu ya kuzingatia na kuonyehsa jinsi vitu visivyo hai vinavyoathiri uhusiano unaozaliwa kwenye nafasi hiyo ya ‚kusubiri tu', yaani ya kutengeneza chai na kutengeneza kazi. Katika mifano yote miwili nafasi hiyo ni nafasi isiyotafsirika iwe wakati au pahala, bali wakati-na-pahala penye fursa za kutengeneza mustakabali maalum.

[13] Mawasiliano ya kibinafsi yaliyotokea tarehe 19 Novemba 2021, mjini Mainz, Ujerumani.

kuwa mseto mtamu – vijana hao hawana umuhimu wala mashiko, yaani hawamata! Jamii inawapinga kwa sababu kazi yao inachukuliwa kana kwamba iko mpakani baina ya ‘kile kilicho sawa, safi, cha kimaadili, cha kitamaduni, cha Kizanzibari’ na ‘kile kinachotisha, kisichojulikana kwa undani, kile ambacho uso wake unakumbusha zamani yenye ukatili wa kikoloni unaotafsiriwa moja kwa moja kwenye ‘ukatili wa kitalii’. Lakini je, mbona tour guides hawachukuliwi hivi? Kazi yao si inawarejesha huko huko mpakani? Pengine utamaduni wa kimseto wa mapapasi haukubaliki kwa sababu una nguvu maalum inayotokana na mshikamano na imani ambayo msingi wake si damu wala dini katika upekee wake, bali urafiki ulioundwa kwa sababu ya nafasi yao ya kikazi na kimaisha (ambayo bila shaka ina uhusiano wa karibu na damu na dini pia), ‘’iliyotokezea’ na ‘kutafutwa’ (ikitegemea nafsi yao), yaani nafasi ya upapasi. Pengine utamaduni huo huo usioingilika kwenye kategoria rasmi yoyote ndio unaotisha na kutikisa serikali inayowapinga kwa sababu ya kutokuwa ‘wa kawaida’ wala ‘wa kikanuni’. Tatu, historia hii inatuelekeza njia maalum ya kuelewa mji, sio kwa mtazamo wa serikali, bali kwa mtazamo wa mji wenyewe. Tujieleze zaidi hapo: serikali ilijaribu kila njia kutekeleza mradi wake maalum unaofuata masimulizi ya ‘mpango mji’ ambao ndio ule ule tangu enzi na enzi; masimulizi hayo yana msamiati pekee wa usafi-usalama-utawala bora-utaratibu-kuzuia-kupanga-kutenga-kusafisha ulio na nia ya kutawala, kuamrisha na kuwa na mamlaka juu ya mji, na wenye/ji wake. Kwa njia hiyo, serikali inachora ramani ya mji wa Zanzibar na kuugawanya kufuata dhana pekee ya uhalali, urasmi, na usawa. Ndivyo serikali inavyoamua nani ni wenyeji na wapi wenyeji wanaruhusiwa ‘kumiliki’ mji ‘walio nao’. Katika ramani hiyo, mapapasi, kama wapo, basi wasiwepo. Yote tuliyowahadithia lakini yanaonyesha ramani tofauti, utasema si Zanzibar! Kwenye ramani hiyo, hakuna uwenyeji wa aina moja, bali uwenyeji wa aina mbalimbali na tofauti. Ramani hiyo inajitokeza ikiwa tu mtazamo hautokei serikalini bali mjini, na haswa kona ya Shangani posta, nafasi yao ya kazi. Ni kwa njia hiyohiyo kwamba kona ghafla inakuwa ofisi na hatuna budi kukubali kuwa ofisi si jengo maalum wala pahala penye majengo fulanifulani, wala njiapanda tu, bali ndiyo jumla ya wahusika (tusisitize, siyo wajihusishao) wote: majengo, mapapasi, wauzaji, wageni, wapitanjia, seremala, magari, hekaheka, sisi, mwendo na mwenendo wao, sauti, vumbi, upepo, na kila kipengele kilichoko au kinachozalishwa konani kikichangia uundaji wake wa kuwa ofisi. Ni hapo ambapo hayo yote yanahusiana (na kuhusishana) kuwa ofisi inazalishwa; ni uhusiano huo unaosababisha kona iwe ofisi. Ni ofisini kwetu hapo kuwa mapapasi wanajipatia uwenyeji, papo hapo ambapo serikali inawazuilia kisheria, isipowafukuza. Ni hapo wanapojipatia nafasi ya kazi, ya kimaisha, ya kuwa na mustakabali, kutokana na nafsi yao, pamoja na yale yote wanayoyakuta konani. Tena ni hapo hapo kuwa maarifa yao yanaunda historia mojawapo ya mji wa Zanzibar inayostahiki kusimuliwa, historia inayomata miongoni mwa nyingi za historia zinazounda na kuundwa na wenyeji Wazanzibari. Nne, tutie mkazo vitu viwili ofisini: kibali na benchi. Kibali chenyewe kina athari yake, kikiwepo na kisipokuwapo: kuwepo kwake kunasaidia kuendesha kazi za kila siku, ila kibali hakitoshi kuunda na kutimiza nafasi ya mapapasi. Kutokuwepo kwake kunawakosesha

mapapasi urasmi na uhalali wa kiserikali, ila kunawawezesha kufanya kazi mpaka leo na kujipatia nafasi katika mji kama wenyeji. Uwenyeji wao unategemea upapasi. Kibali kingalikuwepo, basi mapapasi wangelikuwa tour guide tu, na upapasi ungelififia na uwenyeji wao ungefutwa. Benchi sio kifaa cha kukalia tu, kama ilivyokuwa baraza kuwa si saruji tu, bali benchi linakuwa na maana nyingi zaidi likitizamwa kwenye kazi ya upapasi, yaani kwenye uhusiano na matumizi yake pamoja na masimulizi na vitendo vya mapapasi. Kwa njia hiyo, tunagundua kwamba benchi linasababisha vitu fulani, vitendo fulani na masimulizi fulani kutendewa. Kwa hivyo, uwezo wake huo unatueleweshajinsi upapasi unavyotendeka: upapasi unaundwa kutokana na uhusiano endelevu (kwa maana ya relationality) ambapo mapapasi na benchi, na kila kilichopo ofisini, vina umuhimu na uwezo sawasawa. Pengine ni kutokana na kuchambua ofisi kupitia neno la na ulimwengu wa nafasi kuwa tunapata kuelewa kuwa uundaji wa kona kama ofisi hautegemei mapapasi peke yao, wala kibali peke yake, wala benchi tu peke yake, bali unategemea mkutano, mtangamano, mitagusano na mwingiliano baina ya hayo yote.

Kwenye mazungumzo yetu tulijaribu kuwatafsiria – au bora kuwa*nafsiria*, kama mwananthropolojia M. Yunus Rafiq (2021) anavyotuelimisha, akisisitiza uhusiano wa karibu na mwingiliano baina ya mtu nafsi yake na kitendo cha kutafsiri – nafasi ya upapasi mjini Zanzibar. Tukirejea yale yote yaliyoibuka kutoka katika mazungumzo yetu, tulipokuwa tunawasiliana na mapapasi wengine pia, ni dhahiri kuwa nafasi ina maana na madhumuni mbalimbali ambayo hayatoi tu ishara tofauti ya mji, bali pia yanaathiri jinsi mapapasi wanavyojipatia uwenye-ji wao; na kwa maana hiyo hujipatia pia utambulisho wao pamoja na kujiwezesha kuandika upya historia ya mji wa Zanzibar kwa upande wa kijamii na kiuchumi. Kwa hivyo uwezo wa nafasi haupo tu kwenye semantiki yake, bali pia kwenye uhusishi wa uyakinifu na amali. Ndiyo, nafasi ya upapasi ni pahala, lakini vilevile inauhusiana na nyakati zinazofuata mwendo na mwenendo wa vitu vyote (au vyumbe vyote, vinavyoishi na visivyoishi) vinavyounda ofisi. Nafasi ni bahati, ni fursa, lakini pia hadhi ya kona, vitu ‘vyake’ na watu ‘wake’. Kwa hivyo, badala ya kujaribu kuchambua kila kipengele tunachokumbana nacho konani, tunajihusisha na kona kupitia dhana ya nafasi. Kwa njia hiyo tunafanikiwa kuhisi – kuona-kusikia-kuwa na – mji (na sio kuelewa!), jinsi unavyojitokeza kutokana na kuwepo kwa uhusiano na uhusishi endelevu wa mapapasi na yale yote yaliyomo konani. Kwa maana hiyo, kitendo hicho cha kuwemo konani hakitokezei wakati ‘wake’, bali kina nafasi yake – nafasi ya upapasi – inayobeba yaliyokuwemo zamani pamoja na kutarajia yatakayotokezea siku za mbeleni. Kuchambua nafasi hiyo kunafunua fursa ya kuifafanulia kama kielelezo cha au methodolojia ya kuchambua maneno ya Kiswahili kwa vile yalivyo, lile yanayoliwezesha, pamoja na maana yao. Madhumuni ni kudhihirisha vile maneno si maneno tu – “as if a word could be a word!” (Povinelli et al. 2021: 310) – hayaleti maana tu, bali yana uwezo wa kusababisha, kuunda na kuathiri uhalisia kana kwamba yana uhai (Hussein 1969). Maneno yana uhai maalum, yanabeba vitendo na historia zinazohusiana na vitendo hivyo, vya zamani, vya leo

na vya kesho. Kuchambua maneno ni sawasawa na kuchambua malimwengu, kila neno ni ulimwengu maalum ambao unasubiri kutiliwa maanani kwa vile uswahilini – yaani katika ulimwengu na lugha ya Kiswahili – hatuwezi kugawa maana na kitendo. Nafasi ya upapasi ni mfano mmojawapo unaotuonyesha njia tofauti ya kujaribu kuugusa na kuuhisi mji na uwenyeji unaohusiana nao.

Hivo basi, tunategemea kuwatia ari na moyo kuzikaribisha historia mbalimbali kutoka mjini ambazo hazijasikika. Historia hizo zinaunda nafasi za aina mbalimbali lakini tunadhani hazitiliwi maanani pamoja na kuwa zinatoka uswahilini. Tunabakia kutafakari zaidi kuhusu uhusiano baina ya nafasi na nafsi, kwa kuwa maneno haya yametoka mbali na kurudi uswahilini. Pengine yakawa mamoja sasa – naf(a)si – na kama ni kweli kuwa "ntu huzaa neno, na neno likawa kubwa kuliko ntu" (Hussein 1969: 28), tujiulize hilo neno naf(a)si linabeba nini? Ni nini haswa linalowezesha? Pengine kwa jinsi linavyounganisha maeneo mawili – moja linalogusika, jengine lisilogusika – lina uwezo wa kutusaidia kuchambua uhusiano baina ya mwili wa kibinadamu na miili ya viumbe vingine (vyenye uhai na visivyo na uhai), na kuelewa uhai wenyewe kwa usawa (kwa maana ya justice) zaidi? Si ndo uhusiano – au uwili huo – uliomo katika neno la nafasi uliotuwezesha kukunjua jinsi mbalimbali za kukaribia na kujikaribisha mjini Zanzibar? Tunaondokea hamu ya kujua ukweli wa (na historia ya) aina moja, bali tunakaribisha njia nyingi mbalimbali za kuelewa na kuelezewa uhalisia. Mwishowe kila uhalisia unatokea naf(a)si yake, yaani ujumla wa mitagusano miongoni mwa pahala, wakati, watu na vitu vinavyouunda.

Tuendelee kutafakari…

**Shukrani**

Shukrani zangu za dhati ziwaendee mapapasi wote niliokutana nao na kushirikiana nao maisha yangu, haswa Muchi kwa kuwa na imani kubwa mpaka basi (JahLova!); Bw. Mohamed Ameir Muombwa na familia yake (ninawakumbuka na kuwapenda kila sekunde); Bi. Alessia Lombardo, pamoja na mumewe Omi na mwanangu Safia (yaani…); Bi. Berenike Eichhorn (ulifikiria Nika-kusahahu, ila sijakusahau) na Bi. Nathalie Arnold Koenings (tupo pamoja daima, nakupenda dada); Bi. Susann Ludwig, Bi. Lara Krause-Alzaidi na Bi. Rose Marie Beck (yote hayo yasingaliwezekana bila ya uvumulivu wenu, imani yenu na mabichwa yenu, wah!); Bi. Vanessa Sänger na Bw. Felix Albroscheit (ahsanteni kwa majadiliano, mapendekezo, maoni, mapenzi na msaada wenu); Bw. Kai Kresse na Bw. Lutz Diegner (ahsanteni kwa kuendeleza Baraza la Kiswahili la Berlin na mapenzi yote mliyo nayo) pamoja na washiriki wote wa BaLaKiBe (wazee na vijana, wasomi na marafiki). Mungu awabariki!

*Irene Bahati*

## Marejeleo


A. 2019. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 08 mwezi wa Kumi na mbili, WhatsApp (kwanzia saa nne mpaka saa tano asubuhi hivi).

A. R. A. 2019. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 26 mwezi wa Pili, Forodhani, Mjini Zanzibar.

Basil, Ibrahim, & Amiel Bize. 2018. Waiting Together: The Motorcycle Taxi. Stand as Nairobi Infrastructure. *Africa Today* 65(2): 73-91.

Bissell, William Cunningham. 2011. *Urban Design, Chaos and Colonial Power in Zanzibar*. Bloomington, Indianapolis: Indiana University Press.

Bissel, William Cunningham. 2005. Engaging Colonial Nostalgia. *Cultural Anthropology* 20(2): 215-248.

de Francisco, Christian. 2004. *Courting Modernity: Tradition, Globalization, and the Performance of Masculinity Among the Papasi of Zanzibar*. PhD diss., University of Tulane.

Haraway, Donna J. 2016. *Staying with Trouble. Making Kin in the Chthulucene*. Durham, London: Duke University Press.

Ho, Engseng & Abdul Sheriff (eds). 2014. *The Indian Ocean: Oceanic Connections and the Creation of New Societies*. London: C. Hurst.

Hussein, Ebrahim. 1969. *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

J. 2019. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 29 mwezi wa Saba, Kileleni, mjini Zanzibar.

Ludwig, Susann. 2017. ›Opening up *La Chance*‹ (Un)certainty Among University Graduates in Bamako, Mali. *Dealing with Elusive Futures: University Graduates in Urban Africa*, ed. by Noemi Steuer, Michelle Engeler & Elísio Macamo. Bielefeld: transcript Verlag. pp. 69-88.

Masquelier, Adeline. 2013. Teatime: Boredom and the Temporalities of Young Men in Niger. *Africa* 83(3): 470-491.

M. S. 2018. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 30 mwezi wa Saba, Shangani Posta, mjini Zanzibar.

O. M. 2019. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 24 mwezi wa Saba, Michamvi, kisiwani Unguja.

Povinelli, Elizabeth, Daniela Gandorfer & Zulaikha Ayub. 2021. Mattering-forth: Thinking-with Karrabing. *Theory & Event* 24(1): 294-323.

Prestholdt, Jeremy. 2008. *Domesticating the World African Consumerism and the Genealogies of Globalization*. Berkley, Los Angeles, London: University of California Press.

Rafiq, M. Yunus. 2021. Writing and Translating Ndege Wawili Tena by Mohamed Rafiq into Kiswahili. Wasilisho kwenye warsha ya *TAFSIRI: Siasa ya Kutafsiri na Kujikwamua kutoka kwenye Ukoloni katika Taaluma ya Kiswahili*, tarehe 19-20 mwezi wa Novemba 2021, Chuo Kikuu cha Mainz, Ujerumani.

S. A. 2019. Mahojano na Irene Brunotti ya tarehe 26 mwezi wa Saba, Vuga, mjini Zanzibar.

Sheriff, Abdul. 2010. *The Dhow Culture of the Indian Ocean: Cosmopolitanism, Commerce & Islam*. London: C. Hurst; NY: Columbia University Press.